

RI Executive Office of Health & Human Services  
Rhode Island Medicaid Program  
PO Box 8709  
Cranston, Rhode Island 02920



Mpendwa Mwanachama wa Medicaid,

The Rhode Island Executive Office of Health and Human Services (EOHHS) inaomba usaidizi wako ili kuboresha zaidi huduma yako ya afya. Tuna utafiti mfupi unaochukua dakika 3 hadi 4 wenye maswali yanayolenga kupata maoni yako kuhusu huduma za afya unazopokea kwa sasa. **Maoni yote utakayotoa ni ya siri na hayataathiri manufaa yako ya Medicaid.**

Ili utoe maoni kwa EOHHS, bofya kiungo kilicho hapa chini na ujaze utafiti kufikia **tarehe 31 Mei, 2021.**

Tumeambatisha toleo la karatasi la utafiti huu hapa ambalo unaweza kulijaza na kulituma kwa EOHHS kwa njia ya barua. Unaweza kupata toleo la kielektroniki la utafiti huu, ikiwa ni pamoja na tafiti zingine kwa lugha mbalimbali, kwenye tovuti yetu ya [eohhs.ri.gov](http://eohhs.ri.gov). Changanua msimbo wa QR ulio kwenye barua hii au unaopatikana katika sehemu ya juu ya utafiti kwa kutumia simu yako ya mkononi na ujaze utafiti mtandaoni bila kuhitaji kutuma.

Ni muhimu kupata maoni yako kuhusu huduma za afya unazopokea. Hii ni fursa yako ya kutusaidia. Asante kwa muda wako. Kwa usaidizi wako, tunaweza kukuza mpango bora zaidi wa huduma za afya wa Medicaid.

Wako mwaminifu,  
Womazetta Jones  
Katibu